# Funga kazi

Waandishi Wetu, Mwananchi
mwananchipapers@mwananchi.co.tz

**Dar es Salaam.** Wakati ikiwa imebaki saa chache kwa Watanzania kuamua nani awe diwani, mbunge na Rais, vyama vya siasa vinavyoshiriki uchaguzi mkuu vimejinasibu kuibuka na ushindi kutokana na kazi kubwa waliyoifanya kwenye kampeni.

Kampeni za uchaguzi mkuu utakaofanyika Oktoba 29, zilianza Agosti 28 na zinahitimishwa leo kwa upande wa Tanzania Bara. Zilikuwa siku 61 za vyama kunadi ilani zao kwa njia mbalimbali ikiwemo mikutano na vyombo vya habari.


Wakati Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC), ikieleza maandalizi yamekamilika, Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime katika taarifa yake kwa umma aliwahakikishia wananchi kwamba jeshi hilo limejipanga vizuri kumdhibiti yeyote yule kwa mujibu wa sheria atakayejitokeza ama kwa makusudi au nia ovu kuvunja sheria za nchi ili kuhatarisha amani ya nchi kwa kisingizio chochote kile siku hiyo ya kupiga kura na baada ya kupiga kura.

Pamoja na hayo, baadhi ya huduma mathalani ya usafiri wa mabasi ya mikoani wa kwenda au kurudi Zanzibar -Dar es Salaam zitasimama ili kuruhusu wananchi kwenda kupiga kura.

Uamuzi huo umeelezwa ni sehemu ya mchango wa kampuni za mabasi kuhakikisha abiria na wafanyakazi wake wanatumia haki yao ya kikatiba ya kupiga kura bila vikwazo vya usafiri.

Katikati ya hayo, Ofisi ya Msajili wa Hazina imezitaka taasisi zilizo chini yake kutoa ruhusa kwa wafanyakazi waliojiandikisha nje ya vituo vyao vya kazi ili waushiriki upigaji kura.

Tayari Rais Samia Suluhu Hassan ametangaza Oktoba 29, kuwa siku ya mapumziko ili Watanzania milioni 37.6 waliojindikishaji kwenye Daftari la Kudumu la Mpigakura washiriki kikamilifu huku akiwahakikishia usalama.



Wasimamizi wa vituo vya kupigia kura Jimbo la Kilombero, mkoani Morogoro wakila kiapo jana cha kutunza siri na tamko la kujitoa uanachama wa chama cha siasa baada ya kupewa mafunzo na Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) ya namna ya kutekeleza majukumu yao wanapokuwa kwenye vituo vya kupigia kura siku ya uchaguzi Oktoba 29 mwaka huu. **Picha Hamida Shariff**

"Kauli za kushinda asilimia kubwa ni za kisiasa na kwa kuwa wapo kwenye ushindani lazima waseme hivyo, ingawa katika nchi yetu bado mambo ya uchaguzi hajakaa sawa ili kutuwezesha kujua matokeo kwa uwazi."

Mhadhiri UDSM, Profesa George Kahangwa

"Ni kweli baadhi ya kampuni zimeamua kusitisha safari zake hususani siku ya kupiga kura (Oktoba 29) baadhi ya kampuni zina hofu kwamba abiria watakuwa wachache, hivyo zikaona zisitishe."

Msemaji wa Taboa, Mustapha Mwalongo

## Tambo la vyama

*Mwananchi* imezungumza na baadhi ya viongozi wa vyama 17 vilivyosimamisha wagombea urais kuhusu ya siku 60 za kampeni maeneo mbalimbali nchini huku kila mmoja akieleza kilivyofanya mikutano yake na ushindi wa zaidi ya asilimia 50.

Wagombea hao 17 ni Wilson Peter (ADC), Salum Mwalimu (Chaumma), Abdul Mluya (DP), Yustas Rwamugira (TLP), Saum Rashid(UDP), Mwajuma Mirambo (UMD), Samandito Gombo (CUF) na Samia Suluhu Hassan (CCM).

Wengine ni Twalib Kadege (UPDP), Hassan Almas (NRA), Coaster Kibonde (Makini), Majalio Kyara (SAU), Doyo Hassan (NLD), Daud Mwajojele (CCK), Kunje Ngombale -Mwiru (AAFP), Haji Ambar Khamis (NCCR-Mageuzi), na Georges Busungu wa Ada Tadea.

Wingi wa watu kwenye mikutano yao na wale waliowafuatilia kupitia vyombo vya habari na mitandaoni inawapa jeuri ya kuonesha wanakwenda kuibuka na ushindi. Hata hivyo, wanazuoni wanaeleza wingi wa watu mikutanoni si kigezo cha kuibuka na ushindi.

Katibu Mkuu AAFP, Rashidi Rai alisema chama chao kimefanya mikutano 67 katika mikoa 23, na kupitia mitandao ya kijamii na vyombo vya habari, wamefanikiwa kufikia watu milioni 77, akidai kuwa wamekizidi CCM kwa asilimia kubwa katika kufuatiliwa.

Rai alisisitiza chama chao kinatarajia kushinda uchaguzi wa mwaka huu kwa asilimia 62, ingawa alionya kuwa ikiwa kutakuwa na hila, ushindi wao unaweza kupungua.

ADC kupitia mgombea wake, Wilson Peter alisema amefanya mikutano 91 katika mikoa 26 na kufikiwa na Watanzania milioni 30 moja kwa moja, huku wakisema kuwa milioni 45 walifuatilia kupitia mitandao ya kijamii.

Peter alikadiria aitashinda kwa asilimia 55:"Mikutano yetu kupitia mitandao ya kijamii wamefuatilia watanzania milioni 45 katika mikutano 91 tuliyofanya kwenye mikoa hiyo 26 na matarajio yetu tutashinda kwa asilimia 55."

Katibu Mkuu wa DP, Abdul Mluya alisema amefanikiwa kuwafikia Watanzania wengi kupitia mikutano 105 katika mikoa 22.

Hata hivyo, alisema hawezi kutaja asilimia kamili ya watu waliomfuatilia lakini alionesha matumaini ya kushinda kwa asilimia 68, akisema ikiwa haki itatendeka.

Mgombea wa UDP, Saum Rashid alisema chama chake kinatarajia kushinda kwa asilimia 88, huku akiongeza kuwa wamefanya mikutano 98 katika mikoa 28 ya Tanzania, na mapokezi ya Watanzania kwa chama chao ni makubwa.

"Tumezunguka mikoa 28 kuna baadhi ya mikoa tulifanya mikutano ya hadhara zaidi ya mitatu, sitaki kusema nilifuatilia na idadi gani ya raia ila wapiga kura nimewafikia," alisema.

Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM, Kenan Kihongosi, alisema mgombea wa CCM, Samia amefanya mikutano 114 katika mikoa yote ya Tanzania, huku takwimu za mitandao zikionesha amefuatiliwa mara milioni 164.9 na kuthibitisha kukubalika kwake na umaarufu wa chama hicho.

Alisema zaidi ya watu milioni 25.3 walijitokeza kwenye mikutano ya hadhara, na milioni 57.1 walifuatilia kampeni zao kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.



Mkazi wa jijini Dar es Salaam akipita katika eneo yalipowekwa mahema ikiwa ni matayarisho ya kituo cha kupigia kura katika eneo la Magomeni, jana. **Picha na Ally Mlanzi**

"Sisi CCM katika mikutano ya kampeni tumeweka rekodi kubwa ya mahudhurio kuwahi kutokea tangu kuasisiwa kwa mfumo wa vyama vingi 1992, watu milioni 25.3 wamehudhuria mikutano yetu ya hadhara, watu milioni 57.1 wamefuatilia kampeni zetu kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ndani na nje ya nchi yetu," alisema.

Chama cha Makini, kiliongozwa na mgombea urais, Coaster Kibonde, kimesema kimefanya mikutano mingi nchi nzima, na kuahidi ushindi wa asilimia 72.

UPDP, kupitia mgombea wake Twalib Kadege alisema amefanya mikutano mikoani 17 na kuwa anatarajia ushindi mkubwa, lakini ameongeza kuwa ni jukumu la wapigakura kusema ni asilimia gani atapata.

TLP kupitia Katibu Mkuu wake, Bakari Makame alisema matumaini ya chama chao kupata ushindi wa asilimia 90 inawezekana kutokana na mapokezi mazuri ya wananchi katika mikutano yao 96.

Kulingana na maelezo ya Bakari aliongeza mwitikio wa wananchi kwenye vyombo vya habari pia unathibitisha nguvu ya chama hicho kukubalika kupitia sera zao.

Kwa upande wa chama cha NRA, kupitia mgombea wake, Hassan Almas alisema amewafikia Watanzania kwa njia nyingi, akisema kuwa siasa ni mchakato wa imani, na anatarajia ushindi kupitia nguvu ya Mungu na wapigakura.

## Walichokisema wasomi

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (DSM), Profesa George Kahangwa, alisema asilimia hizo wanazobainisha ni siasa hazina uhalisia wowote





huku akisema kuwa na umati mkubwa katika mkutano wako haimaanishi watakupigia kura.

"Wakati mwingine umati mkubwa wa watu kujitokeza hauna uhalisia moja kwa moja kwenye matokeo ya kura, isipokuwa kuna watu wanakuja hawana namna wanakuja kukupa matumaini kama wapo na wewe lakini kura anaenda kupigiwa mwingine," alisema.

Kulingana na Profesa Kahangwa alifafanua maudhirio ya watu wengi katika mikutano yanaamuliwa na vitu vingi kwanza wapo wanaoenda kwa sababu ya hiyari yao kumsikiliza mgombea, lakini wapo walioshawishiwa kwa kubeba kwenye vyombo vya usafiri.

Alisema makundi makubwa yanaweza kuonesha ni kwa kiwango gani unawafuasi wengi, lakini si lazima wote waliohudhuria watakupigia kura, kwa hiyo huwezi kujihakikishia watakupigia kura.

"Wapo wanaoweza kuamua kumpigia kura mtu mwingine, wapo miongoni mwao hawatapiga kura kwa sababu mbalimbali mathalani hawakujiandikisha au mambo mengine binafsi," alisema Profesa Kahangwa.

Pia alisema kuna baadhi ya vyama vimekuwa vimeenda kupiga kampeni kwenye masoko na hata kwenye mitandao kuna wanaokuangalia katika kuongeza idadi pekee kuna kuwa hakuna uhalisia.

Mchambuzi wa masuala ya siasa, Abdulkarim Atiki, alisema takwimu hupingwa kwa takwingu ingawa amedai CCM katika mchuano huo haina mshindani wa kweli hivyo uhakika wa kushinda ni mkubwa kwao.

"Matokeo kuwa tofauti ni labda wananchi waamue au wawe wamekichukia chama kweli ndipo kura waelekeze sehemu nyingine, lakini ilivyo CCM ni kama Yanga kwenye ligi hawana mshindani wa kushindana naye,"alisema

**17**
Idadi ya wagombea kat8ika nafasi ya urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**Mil 37.6**
Idadi ya wananchi waliojiandika kupiga kura katika uchaguzi wa mwaka huu.

Si hivyo tu Atiki alisema CCM kina mengi ya kueleza kwa wananchi kwa kuzingatia wapo madarakani kwa muda mrefu na wanaleta huduma za kijamii kwa wananchi hivyo wanaweza kueleza wamefanya mambo gani.

## 'Wafanyakazi waruhusiwe'

Katika hatua nyingine, Ofisi ya Msajili wa Hazina imezitaka taasisi zilizo chini yake kutoa ruhusa kwa wafanyakazi waliojiandikisha nje ya vituo vyao vya kazi ili washiriki katika uchaguzi huo.

Mkurugenzi wa Usimamisi Mashirika ya Kibiashara kutoka Ofisi ya Msajili wa Hazina, Lightness Mauki alisema ni vyema kuhakikisha watumishi wote wa umma waliopo katika taasisi na mashirika ya umma kote nchini wanatumia haki yao ya msingi ya kikatiba kwa kushiriki kikamilifu katika uchaguzi mkuu.

## Huduma ya usafiri

Wakati Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (Taboa) ikieleza sababu za baadhi ya kampuni kusitisha safari zake kati ya kesho Oktoba 28 hadi 30, Chama cha Kutetea Abiria kimesema sababu hizo hazina mashiko kwani kila mtu ana shida zake za kijamii, kifamilia,misiba na au ugonjwa.

Baadhi ya kampuni za usafirishaji wa barabara na nyingine za majini zimetangaza kusitisha safari zake kati ya kesho Oktoba 28, hadi 29 na nyingine kwenda hadi Oktoba 30.

Baadhi ya kampuni za mabasi yanayofanya safari zake kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza, Tarime (Mara), Kilimanjaro, Arusha, Tabora, Mpanda (Katavi), Bukoba, Karagwe (Kagera), Kigoma na baadhi ya mikoa imetangaza kutosafirisha abiria Oktoba 29, siku ambayo Watanzania watapiga kura.

Msemaji wa Taboa, Mustapha Mwalongo alisema huo si msimamo wa Taboa, isipokuwa ni kampuni mojamoja zimeamua kutofanya safari siku hiyo.

"Kama nilivyosema huo si msimamo wa Taboa, ni kampuni moja moja, zipo baadhi zimepunguza ruti, mfano mtu anapeleka gari tano Mbeya, siku hiyo ana hofu kama abiria hawatokuwepo, hivyo anapunguza na kusalia na ruti moja," alisema.

Alisema wamiliki wa mabasi wanaamini uchache wa abiria siku hiyo, hivyo wamelazimika kupunguza ruti na wengine kusitisha safari ili kutoa mwanya kwa Watanzania kushiriki kikamilifu kupiga kura.

Hata hivyo, Katibu wa Chama cha kutetea abiria, Hashim Omary alisema sababu za wamiliki wa mabasi ni za nidhamu ya uoga ambazo hazina mashiko.

"Huko ni kukiuka sheria za usafirishaji, kwani unaweza usipeleke gari na watu wasipige kura, zingekuwa na mashiko kama Serikali ndiyo ingekuwa imewambia wasitishe, lakini kama ni uamuzi binafsi, hizo ni sababu ambazo hazina mashiko," alisema.

Alisema kila mtu anaposafiri huwa na sababu zake za msingi, wengine ni za ugonjwa, mwingine anawahi sehemu ambayo hawezi kuacha kwenda.

"Sasa unaachaje kumpeleka kwa sababu ya kupiga kura? Sidhani hata Serikali inaunga mkono hili, hayo ni mawazo yao ya uoga kwamba wataunguza mafuta.

"Kama chama cha kutetea abiria tunaamini siku hiyo abiria wapo kama kawaida, kwani kila mtu ana shida zake za kijamii,kifamilia, misiba wagonjwa, kusitisha safari hakuna mashiko," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (Latra), Johansen Kahatano alipoulizwa juu ya baadhi ya mabasi kusitisha huduma za usafiri, alisema amezungumza na baadhi ya wamiliki na kujua sababu.

"Mmoja kasema ni sababu ya usalama, lakini tayari polisi walishatoa taarifa kuhakikisha hali ya usalama nchini siku ya uchaguzi hilo sio tatizo, na tumewambia na chama chao kuhusu hilo.

"Baadhi ya wamiliki walisema wao wataendelea kutoa huduma kama kawaida, hakuna shida, ni wachache sana ambao wamesitisha, lakini ni kwa sababu zao tu," alisema.

CamScanner